

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA SABA**

**14 NOVEMBA, 2018**

## **MKUTANO WA KUMI NA TATU**

### **KIKAO CHA SABA – TAREHE 14 NOVEMBA, 2018**

#### **I. DUA:**

Saa 3.00 asubuhi, Mhe. Dkt. Tulia Ackson Naibu wa Bunge, alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

#### **MAKATIBU MEZANI:**

- i. Ndg. Lawrence Makigi
- ii. Ndg. Asia Minja
- iii. Ndg. Ruth Makungu

#### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Hati zifuatazo zitawasilishwa mezani:-

- (i) Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake ;
- (ii) Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama aliwasilisha Maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio hilo;
- (iii) Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliwasilisha Maoni ya Upinzani kuhusu Azimio hilo;
- (iv) Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Mezani Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*);
- (v) Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aliwasilisha Mezani Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika;

- (vi) Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango aliwasilisha Mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

Swali Na. 85: Mhe. Maryam Salum Msabaha

Nyongeza: Mhe. Maryam Salum Msabaha  
Mhe. Ruth Hiyob Molel  
Mhe. Peter Simon Msigwa

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na. 86: Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda

Nyongeza: Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda  
Mhe. Mundwe Abdallah Tambwe

#### **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Swali Na. 87: Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni

Nyongeza: Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni  
Mhe. Timotheo Paul Mnzava  
Mhe. Willy Qambalo Qulwi  
Mhe. Balози Adadi Rajab  
Mhe. Mariam Nassor Kisangi

Swali Na. 88: Mhe. Anthony Calist Komu

Nyongeza: Mhe. Anthony Calist Komu  
Mhe. Lucy Fidelis Owenya  
Mhe. Cecil David Mwambe

**WIZARA YA KILIMO:**

Swali Na. 89: Mhe. David Ernest Silinde

Nyongeza: Mhe. David Ernest Silinde  
Mhe. Frank George Mwakajoka

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Swali Na. 90: Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete

Nyongeza: Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete

Swali Na.91: Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa

Nyongeza: Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa

Swali Na. 92: Mhe. Jasson Samson Rweikiza

Nyongeza: Mhe. Jasson Samson Rweikiza  
Mhe. Ezakiel Almas Maige

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Swali Na. 93: Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi

Nyongeza: Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi

Swali Na. 94: Mhe. Ritta Enespher Kabati

Nyongeza: Mhe. Ritta Enespher Kabati

Swali Na. 95: Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata kny: Ignas Aloyce Malocha

Nyongeza: Mhe. Ignas Aloyce Malocha

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Swali Na. 96: Mhe. Zacharia Paulo Issaay

Nyongeza: Mhe. Zacharia Paulo Issaay

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Swali Na. 97: Mhe. Silafu Jumbe Maufi

Nyongeza: Mhe. Silafu Jumbe Maufi

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Swali Na. 98: Mhe. Maulid Said Mtulia

Nyongeza: Mhe. Maulid Said Mtulia

**MATANGAZO WAGENI**

- (i) Wageni waliokuwa Jukwaa la Spika Viongozi wa Umoja wa Vyama Taifa – CCM walitambulishwa;
- (ii) Wageni 4 wa Mh. Mwakyembe kutoka Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania;

(iii) Wageni walitambulishwa.

#### KAZI

- (i) Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara watakuwa na Kikao mara baada ya kuahirisha Bunge – Msekwa Dispensary;
- (ii) Semina kwa Wabunge Wanawake Ukumbi wa Msekwa saa 7.00 Mchana;
- (iii) Wabunge Waislam watakuwa na Kikao saa 7.00 Mchana Ukumbi wa Msekwa;
- (iv) Wabunge Wakatoliki kushiriki ibada ya Misa Ukumbi wa Msekwa B saa 7.00 baada ya kusitishwa Bunge;
- (v) TEP Ltd wanafanya maonyesho ya vitabu jengo la Utawala.

#### IV. HOJA ZA SERIKALI:

##### MAAZIMIO

- (i) Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake (*The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and their Destruction*) wa Mwaka 1972.

- (ii) Waziri wa Fedha na Mipango:

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*).

## **I. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

- (a) Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliwasilisha Hotuba ya Wizara kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake wa mwaka 1972;
- (b) Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama aliwasilisha Maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio hilo;
- (c) Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliwasilisha Maoni ya Upinzani kuhusu Azimio hilo;

## **II. WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO**

- (a) Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Mezani Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*);
- (b) Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aliwasilisha Mezani Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika;
- (c) Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango aliwasilisha Mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika.

Wafuatao walichangia Maazimio kama ifuatavyo:-

- |                                      |   |         |
|--------------------------------------|---|---------|
| 1. Mhe. Ally Saleh Ally              | - | CUF     |
| 2. Mhe. Richard Philip Mbogo         | - | CCM     |
| 3. Mhe. Balozzi Adadi Mohamed Rajabu | - | CCM     |
| 4. Mhe. Saed Ahmed Kubenea           | - | CHADEMA |
| 5. Mhe. Albert Obama Ntabaliba       | - | CCM     |

6. Mhe. Salum Mwinyi Rehani - CCM

### **III. KUSITISHA BUNGE:**

Saa 7.00 mchana Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson alisitisha Bunge hadi saa 11.00 Jioni.

### **IV. BUNGE KUREJEA:**

Saa 11.00 Jioni Bunge lillirejea.

Mjadala kuhusu Maazimio uliendelea na Waheshimiwa Wabunge wafuatao walichangia:-

- |                                   |   |         |
|-----------------------------------|---|---------|
| 7. Mhe. Ruth Hiyob Mollel         | - | CHADEMA |
| 8. Mhe. Augustino Manyanda Masele | - | CCM     |
| 9. Mhe. Jasson Samson Rweikiza    | - | CCM     |

### **KUHITIMISHA HOJA**

1. Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alihitimisha Hoja kwa kutoa maelezo ya ufafanuzi kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu Pamoja na Uangamizaji wake wa mwaka 1972, katika maeneo ambayo Wabunge walitoa maoni na ushauri kwa Serikali wakati wa kuchangia Azimio hilo.

Hoja ilitolewa na kuafikiwa na Bunge Mhe. Naibu Spika aliwatakiwa kila la heri Serikali katika utekelezaji wa Azimio hilo pamoja na kuzingatia maoni ya Wabunge.

2. Waziri wa Fedha na Mipango alihitimisha Hoja yake kwa kutoa maelezo ya ufafanuzi kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*).

Hoja ilitolewa na kuafikiwa na Bunge.



Mhe. Naibu Spika alimpongeza Waziri wa Fedha kwa kuleta Azimio hilo na kuomba Serikali ikafanyie kazi maoni na mapendekezo ya Wabunge kuhusu Azimio hilo.

Pia aliomba Serikali kuangalia Sheria na Azimio kama vitaendanan na ikibidi Serikali ilete marekebisho ya Sheria ya takwimu Bungeni ili Sheria iendane na Azimio hilo.

## **V. AZIMIO:**

Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu

Azimio la Bunge la Kumpongeza Dkt. John Pombe Joseph Mafuguli, Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada na maamuzi mbalimbali ya kuwainua Wananchi, Wanyonge hasa Wakulima wa Korosho na Wakulima wa Mazao mengine.

Hoja ilitolewa na kuamuriwa. Wafuatao walichangia:-

- |                                      |   |         |
|--------------------------------------|---|---------|
| 1. Mhe. Hassan Elias Masala          | - | CCM     |
| 2. Mhe. Riziki Said Lulida           | - | CUF     |
| 3. Mhe. Daimu Iddi Mpakate           | - | CCM     |
| 4. Mhe. Godbless Jonathan Lema       | - | CHADEMA |
| 5. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi | - | CCM     |
| 6. Mhe. Pascal Yohana Haonga         | - | CHADEMA |
| 7. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia      | - | CCM     |
| 8. Mhe. Ezekiel Magolyo Maige        | - | CCM     |
| 9. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi       | - | CCM     |
| 10. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri     | - | CCM     |
| 11. Mhe. Sikudhani Yassin Cchikambo  | - | CCM     |
| 12. Mhe. Mohamed Zuberi Kuchauka     | - | CCM     |

Mtoa Hoja Mhe. Elibariki Kingu alihitimisha Hoja yake.

Kiti kilielekeza Hoja iliyochapwa ndiyo itaingia Hansard, Hoja iliamuriwa na kuafikiwa.

Naibu Spika alimpongeza Mtoa Hoja na kuomba Serikali kufanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Wabunge. Alimpongeza Rais kwa uamuzi aliochukuwa.

Chief whip awataarifu Halmashauri kuhusu makato yatakayofanyika ili kuwa na ujumbe unaofanana kwa wananchi.

## TANGAZO

Cocktail party katika viwanja vya Bugne itafanyika kesho mara baada ya kuahirisha Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote waliombwa washiriki. Aidha, Wabunge waliombwa kutoegesha magari eneo hilo.

## **VI. KUAHIRISHA BUNGE:**

Saa 1.45 usiku Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Naibu Spika) aliahirisha Bunge mpaka kesho Alhamisi tarehe 15/11/2018 saa 3.00 Asubuhi.